KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA

AL-HUDAA [UONGOFU]

الهدى

25/= Ksh

Volume 25, Issue 1

22nd Ramadhaan 1433

10th August, 2012

WASILIANA NASI

SIMU (+254) 721473181
Mombasa, Kenya
E-MAIL Info@qssea.net
Web Site: http://www.qssea.net

YALIYOMO KATIKA JARIDA LA WIKI HII

SIKU 10 ZA MWISHO ...	1	2
NI LINI USIKU WA ...	2	3
I'TIKAAF NA HUKMU ...	3	4

HABARI ZA MAZINGIRA YA WAISLAMU KWA MUKHTASAR

Vyama visokuwa vya dini vyaongoza Libya

Ishara za awali za matokeo ya uchaguzi wa mwanzo wa taifa kufanywa Libya kwa karibu nusu karne, zinaonesha kuwa muungano wa vyama visivokuwa vya kidini, unaongoza kwenye majimbo muhimu, pamoja na Tripoli na Benghazi.

Afisa wa daraja ya juu katika muungano wa vyama, uitwao National Forces Alliance, alisema ripoti za awali zinaonesha kuwa wao wanaongoza katika uchaguzi huo uliofanywa Jumamosi, kauli ambayo imethibitishwa na kiongozi mmoja wa chama kinachowapinga, cha Islamist Justice.

Maafisa wa uchaguzi wanasema, matokeo rasmi hayatajulikana kwa siku kadha.

Kati ya viti 200 vya bunge, vyama vya siasa vitapata viti 80 tu. Vilivyobaki vitakuwa vya wajumbe wanaojitegemea. **[BBC London]**

SIKU 10 ZA MWISHO ZA MWEZI WA RAMADHAAN

Na: Shaykh 'Abdullaah Ibn Saalih Al-Fawzaan

Amesema bibi 'Aa'ishah (رضي الله عنها): "Zifikapo siku kumi za mwisho za mwezi (wa Ramadhaan), Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akitumia wakati wake kwa ibaada, akiwaamsha wake zake (wakati wa usiku), akijikaza na kujifunga Izaar (kibindo) yake vyema." [Al-Bukhaaree (4/269) na Muslim (1174)]

Hadeeth hii ni dalili ya kutosha yakwamba siku kumi za mwisho za Ramadhaan zina fadhla maalum kuliko siku zozote nyengine (zilizojumlishwa), ambazo ndani yake mtu huongeza kufanya ibaada ya utwi'ifu, kama vile kuswali, kufanya Dhikr na kusoma Qur'an. 'Aa'ishah (رضي الله عنها) amemsifu Mtume wetu katika kuwajibika, Muhammad (صلى الله عليه وسلم), kwa sifa Nne:

1. Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akiutumia usiku wake kwa ibaada", kwa maana ya alikuwa halali wakati huo. Kwahiyo, alikuwa (صلى الله عليه وسلم) akikesha usiku mzima kwa ibaada na alikuwa akiihuisha roho yake kwa kuutumia usiku wake kwa kukesha. Hii ni kutokana na ukweli yakwamba nduguye kifo ni kulala.

Maana ya "kuutumia usiku wake" ni kwamba alikuwa (صلى الله عليه وسلم) akiutumia wakati wote huo kwa Qiyaam (swala ya usiku) na kutekeleza vitendo vya ibaada kwa ajili ya Allaah, Mola wa walimwengu wote. Ni lazima tukumbuke yakwamba siku kumi za mwisho za Ramadhaan zimewekwa na idadi zake zinahesabika. Ama kuhusu yaliyopokewa kuhusiana na kukatazwa kutumia usiku mzima kwa kuswali, kulikotajwa katika hadeeth ya 'Abdullaah ibn 'Amr, basi ni kuhusiana na mtu mwenye kufanya hivyo kwa kuendelea bila ya kukosa kwa mwaka mzima.

2. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa "akiwaamsha jamii yake" ikimaanisha alikuwa akiwaamsha wake zake waliotakasika., mama zao waumini, ili nao wapate kushiriki katika kufaidika na yaliyo mazuri, Dhikr na vitendo vya ibaada katika wakati huu uliobarikiwa.

3. Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) "akijikaza" kwa maana yakwamba alikuwa akijihifadhi na kung'ang'a katika kufanya ibaada, akijiongezea ziyada katika 'amali zake kuliko aliyowahi kuyatenda katika siku ishirini za mwanzo (za Ramadhaan). Alifanya hivyo kutokana na sababu yakwamba usiku wa Qadr hutokea katika masiku hayo (kumi ya mwisho).

4. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akijikaza na kujifunga Izaar (kibindo) yake vyema kwa maana yakwamba alikuwa akijipinda na kupambana na nafsi yake katika kufanya ibaada. Vilevile inasemekana yakwamba maana yake ni Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akijiepusha na wanawake. Hili laonekana kuwa ndilo la sawa kwani limeafiki yaliyotajwa hapo awali na kwa hadeeth ya Anas: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akilikunja godoro lake na kujiepusha na wanawake (yaani; wake

(Endelea kwenye Uk. 2)

EHE NDUGU YANGU!!

ZINDUKA!!

"FUNGUA SAUMU USIFUNGUE MUADHINI" !!

SISI HATUFUNGUI MUADHINI KWA SABABU MUADHINI HAUFUNGWI BALI TWAFUNGUA SAUMU KWA SABABU TWAFUNGA SAUMU.

(Endelea Kutoka Uk. 1)

zake).” [Angalia katika Lataa'if-ul-Ma'aarif, Uk. 219]
Vilevile, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifanya ‘Itikaaf katika siku kumi za mwisho za Ramadhaan na mtu aliye kwenye hali ya kufanya Itikaaf atakatazwa kuingiliana ki-mapenzi na wake zake. Kwahivyo, Ewe ndugu yangu Muislamu, jitahidi uwe na tabia kama hizi. Na uzihifadhi swala zako wakati wa usiku mkubwa (tahajjud) pamoja na Imaam katika Swala za Taraweeh (inayoswaliwa katika nyakati za usiku wa mapema), ili kujitolea kwako kwa juhudi katika siku hizi kumi za mwisho zipate kushinda zile siku ishirini zilizotangulia. Na ili upate kujivunia na sifa ya “kuutumikia usiku kwa ibaada” kwa kuswali.
Na ni lazima uwe na subira katika kumtwi’i Allaah, kwani kwa hakika, swala ya tahajjud (ya usiku) ni ngumu, lakini malipo yake ni makubwa. Wallaahi, ni fursa kubwa sana katika maisha ya mtu na kuitumia ni jambo lenye kuleta faida, kwa mwenye kuafikiwa na Allaah. Na mtu hajui iwapo pengine atapata mojawapo ya malipo mengi ya Allaah wakati wa swala ya usiku, hivyo basi, ikawa ni jambo la usaidizi kwake katika ulimwengu huu na kesho Akhera. Watu wema wa Ummah huu walikuwa wakirefusha swala zao za usiku, kwa kujipinda nafsi zao. Amesema As-Saa’ib ibn Yazeed: “Umar ibn al-Khattaab alimuamrisha Ubay bin Ka’ab na Tameem ad-Daaree kuwaswalisha watu raka’at Kumi na Moja. Msomaji alikuwa akisoma aya mia moja, kiasi cha kwamba ilitubidi kuegemea fimbo zetu kutokana na kisimamo kirefu. Na wala hatukusimama (hatukukoma) mpaka ilipofika sehemu za mwanzo za Alfajiri.” [Angalia al-Muwatta, Vol. 1, Uk. 154].
Amepokea Abdullaah Ibn Abee Bakr: “Nilimsikiya babangu (yaani; Abu Bakr) akisema: ’Wakati wa Ramadhaan, tulikuwa tukimaliza (swala ya usiku) kwa kuchelewa na tukawa tunawaharakisha wafanyi kazi watuletee chakula (au Daku) kwa kuchelea yakwamba huwenda Alfajiri ikatuingilia.” Muwatta cha Imaam Maalik, Vol. 1, Uk. 156. Kuna sampuli mbili za mapambano ya Roho ambayo waumini hupambana nayo wakati wa Ramadhaan: kupambana wakati wa mchana na kufunga na kupambana wakati wa usiku kwa Qiyaam (swala ya usiku). Kwahivyo yoyote mwenye kuyakusanya haya mambo mawili na kutekeleza haki zake, basi atakuwa ni miongoni mwa wenye subira - Wale watakaopewa malipo yao kwa ukiamilifu bila ya kupunguziwa kitu.” [Surat az--Zumar (39):10].
Hizi Siku kumi ni sehemu ya mwisho wa mwezi na vitendo vya mtu hutegemea juu ya vitendo vyake vya mwisho. Kwahivyo, pengine ataupata usiku wa al-Qadr, haliyakuwa amesimama kwa swala kwa ajili ya Allaah na kwahivyo akasamehewa madhambi yake yote yaliyotangulia asamehewe. Na mtu ni lazima ahamasishe na kuhuisha na kuwahimiza jamii yake watekeleze vitendo vya ibaada, hususan katika zama hizi tukufu ambamo hakuna atakaepuuza isipokuwa atakuwa amenyimwa. Kilicho kikubwa zaidi kuliko jambo hilo ni kwamba, wakati watu wanapokuwa wanaswali na kuswali Tahajjud, baadhi ya watu hupoteza wakati wao kwenye mikusanyiko iliyokatazwa na vitendo vya madhambi. Kwa hakika hii ni hasara kubwa. Twamuomba Allaah atuhifadhi. Kwahivyo, kujiingiza kwenye hizi siku za mwisho ina maana ya kuingia kwenye mapato ya faida kutokamana na vitendo vizuri katika yaliyobaki ya mwezi mzima. Kutokamana na mas’ala yenye bahati mbaya ni kuona yakwamba baadhi ya watu hufanya matendo mazuri kwa wingi, kama vile kuswali na kusoma Qur’an, kwenye sehemu za mwanzo za mwezi huu, lakini mara alama za machofu na kuishiwa huanza kujitokeza kwao baadae, hususan siku kumi za mwisho wa mwezi wa Ramadhaan ziingiapo. Na haya licha ya hizi siku kumi za mwisho zenye kisimamo kirefu kuliko za mwanzo. Kwahiyo, inampasa mtu ahifadhi katika kupambana na kujipinda na kuongeza ibaada zake unapokurubia kumalizika mwezi. Na ni lazima tutambue kwenye fahamu zetu yakwamba vitendo vya mtu hutegemea mwisho wake.

NI LINI USIKU WA Al-Qadr?

NA: MASHEIKH MUHAMMAD NAASIR UD-DEEN AL-ALBAANI NA IBN AL-’UTHAYMEEN (رحمهم الله)

Usiku wa Al-Qadr hutokea kwenye masiku kumi ya mwisho wa mwezi wa Ramadhaan, kwenye usiku usio gawika kwa mbili (yaani; 21st, 23rd, 25th, 27th or 29th). Hatahivyo, wanavyuoni nwamekhitilafiana iwapo siku yenyewe ni makhsusi iliyowekwa miongoni mwa haya masiku katika kila mwaka ikiwa inakuwa ni yenye kubadilika kila mwaka.

Yafuatayo ni baadhi ya matamshi ya wanavyuoni wetu wawili wakubwa; Muhammad Ibn Saalih Al-'Uthaymeen and Muhammad Naasir-ud-Deen Al-Albaanee (رحمهم الله).

Usiku wa Al-Qadr Ni Siku Maalum:

[Imaam Al-Albaanee katika Kitaab chake, Qiyaam Ramadaan (Uk. 18-19)]: Usiku ulio bora katika mwezi wa Ramadhaan ni usiku wa Al-Qadr, kutokana na hadeeth ya Mtume: "Yoyote mwenye kuswali swala ya usiku katika usiku wa Al-Qadr kwa Imaan iliyo thabiti na akitarajia kupata malipo, atasamehewa madhambi yake yote yaliyotangulia (yaliyopita).” Kulingana na rai yenye nguvu zaidi, ni katika usiku wa Ishirini na Saba. Ahaadeeth nyingi zinaafikiyana na kauli hii, ikiwemo hadeeth ya Zurr Ibn Hubaysh aliyesema: "Nilimsikiya Ubay Bin Ka'ab (رضي الله عنه) akisema, pindi alipoambiwa yakwamba 'Abdullaah Ibn Mas'ood (رضي الله عنه) amesema "Yoyote atakaeswali swala ya usiku (katika kila usiku) kwa mwaka mzima, atakuwa ni mwenye kuupata usiku wa Al-Qadr.” Akasema (Ubay Bin Ka'ab): Allaah na Amrehemu, niya yake ilikuwa ni kwamba watu wasilemae wakategemea usiku mmoja tu (peke yake). Naapa kwa Yule ambaye hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, kwa hakika ni katika mwezi wa Ramadhaan. Na Wallaahi, mimi najua ni katika usiku gani. Ni katika usiku ambao Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipotuamrisha tuswali swala ya usiku. Ni katika usiku wa Ishirini na Saba. Alama yake ni kwamba Jua huchomoza katika siku ifuatayo kutokana na muangaza wa asubuhi bila ya miyale.” Kwenye riwaya moja hii iliinuliwa na kufanywa kuwa ni maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم):
1.**Usiku wa al-Qadr unahitaji kutafutwa:** [Imaam Muhammad Ibn Saalih Al-'Uthaymeen katika kitabu chake Majaalis

Shahr Ramadaan (Uk. 106-107)]: Usiku wa al-Qadr uko katika siku kumi za mwisho za mwezi wa Ramadhaan, kutokana na hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Utafuteni usiku wa al-Qadr katika siku kumi za mwisho za mwezi wa Ramadhaan." Na iko karibu na siku saba za mwisho, kutokana na hadeeth ya Ibn Umar (رضي الله عنه) yakwamba: "Baadhi ya watu miongoni mwa Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) waliuona usiku wa al-Qadr wakiwa usingizini katika siku saba za mwisho za mwezi wa Ramadhaan. Basi akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Mimi naona yakwamba ndoto zenu nyote zinaafikiyana yakwamba (huo usiku wa al-Qadr) ni katika siku Saba za mwisho. Kwahivyo yoyote atakae na autafute katika siku Saba za mwisho." Na vilevile imetokana na hadeeth katika Muslim kutoka kwa Ibn Umar (رضي الله عنه) yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Itafuteni kwenye Siku kumi za mwisho. Lakini iwapo mmoja wenu atadhoofika hali yake au atashindwa, basi usiziwache siku Saba zilizobaki zimshinde." Miongoni mwa Siku Saba za mwisho, imekurubia zaidi na Siku Ishirini na Saba kutokana na hadeeth ya Ubay Bin Ka'b (رضي الله عنه) aliyesema: "Wallaahi, mimi naujua ni usiku upi, ni katika usiku ambao Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipotuamrisha kutekeleza swala ya usiku. Ni katika usiku wa Ishirini na Saba." Usiku wa al-Qadr haukuhusishwa katika usiku mmoja maalum kila mwaka, bali, hubadilika mara kwa mara. Kwahivyo katika mwaka mmoja huwenda ikawa ni kwenye usiku wa Ishirini na Saba kwa mfano, na kwenye mwaka mwengine inaweza ikawa ni kwenye usiku wa Ishirini na Tano, kulingana na Hikma yake Allaah na Mapendelewa Yake. Yenye kutuelekeza sisi kwenye haya ni hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Utafuteni kwenye usiku wa zitakapobaki siku Tisa, zitakapobaki siku Saba, na zitakapobaki siku Tano (yaani;. 21st, 23rd, na 25th mtawalia bila ya kutajwa usiku wa 27th)." Amesema al-Haafidh Ibn Hajr kwenye Kitabu chake Fat-hul-Baaree: "Rai yenye nguvu mno ni kwamba usiku wa al-Qadr unapatikana katika siku kumi za mwisho (siku zisizoweza kugawanyika kwa mbili) na kwamba hubadilika mara kwa mara." Allaah alificha 'ilmu ya kutokeza kwake kwa waja wake kutokana na Rehma Yake ili waweze kujiongezea vitendo vyake katika kuutafuta (usiku huo) katika siku hizo zenye heshima kubwa, kwa kuswali, kufanya Dhikr, kuomba Du'a. Kwahivyo hukuwa na kuongezeka kujikurubisha kwa Allaah na Malipo yake. Na vilevile (Allaah) aliifanya ikajificha kutokana na wao na kuwa ni kama mtihani wao wa kumbainisha miongoni mwao anayepambana na kufanya bidii aipate na ni yupi aliye mvivu na asiyejali. Hii ni kwa sababu yoyote anayedumu daima katika kupambana na akajipinda nafsi yake katika kuutafuta na kuutendea kazi yake. Na pengine Allaah huwaeleza kwa kuwatambulisha wakati wa kutokea kwake kwa baadhi ya waja wake kwa njia ya alama na ishara, ambao mtu anaweza kuona. Kama ambavyo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivyo ona alama zake yakwamba atakuwa ni mwenye kusujudu ndani ya matope katika mapambazuko yake ya siku iliyofuata. Kwahivyo ikanyesha katika usiku huo, nae akaswali asubuhi iliyofuata ndani ya maji ya mvua."

I'TIKAAF NA HUKMU ZAKE

NA: SHEIKH MUHAMMAD NAASIR UD-DEEN AL-ALBAANI (رحمه الله)

INAPOTUMIKA:

'Itikaaf (kujitenga kando ndani ya msikiti) ni kitendo kilichohimizwa katika mwezi wa Ramadhaan na hata katika siku nyenginezo za mwaka mzima. Asili yake inapatikana katika maneno ya Allaah pindi aliposema: "… haliyakuwa munafanya I'tikaaf kwenye Misikiti." Na vilevile kuna ahaadeeth nyingi zilizo swaheeh kuhusu I'tikaaf ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na riwaya za ma-Saaf kuhusiana na hayo. Zote hizo zimetajwa katika Musannaf za Ibn Abee Shaybah na Abdur-Razzaq. Imepokewa hadeeth swaheeh yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alifanya I'tikaaf katika siku kumi za mwisho za Shawwal, na kwaqmba 'Umar alimwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Mimi niliweka nadhiri (kwa Allaah) katika siku za Jaahiliyyah yakwamba nitafanya I'tikaaf kwa usiku mmoja katika Masjid ul-Haraam, (Sasa Jee nifanye?) Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu: "Tekeleza nadhiri yako." Kwahivyo akafanya I'tikaaf kwa siku moja.

KUITEKELEZA I'TIKAAF KATIKA MWEZI WA RAMADHAAN IMETHUBUTU:

Kuitekeleza I'tikaaf katika mwezi wa Ramadhaan ni jambo lililothubutu kutokana na hadeeth ya Abu Hurairah (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alifanya I'tikaaf kwa siku kumi kila ifikapo mwezi wa Ramadhaan, lakini ulipofika mwaka ambao aliokufia, alifanya I'tikaaf kwa siku Ishirini." Wakati mzuri wa kuitekeleza I'tikaaf ni katika sehemu za mwisho za Ramadhaan kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifanya I'tikaaf wakati wa siku kumi za mwisho za Ramadhaan mpaka Allaah (سبحانه وتعالى) alipoichukuwa roho yake (kufa kwake).

HUKMU ZAKE:

Utekelezaji wake haukuwekwa katika Sheriya isipokuwa ifanyike kwenyeMasaajid, kutokana na alivyosema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na wala musifanye nao (wake zenu) tendo la kimapenzi munapokuwa kwenye I'tikaaf katika Masaajid."** Soorat-ul-Baqarah (2):187. Imaam al-Bukhaari ameitumia aya hii kama dalili ya tuliyoyataja hapo juu. Al-Haafidh Ibn Hajar amesema: "Nukta ya ushahidi inayopatikana katika aya hii ni kwamba lau kama ingelikuwa ni sawa kufanya I'tikaaf mahali kokote pasipokuwa kwenye msikiti, basi makatazo ya kufanya kitendo ya mapenzi hayangelitajwa makhsusi, kwa sababu kitendo cha kuingiliana kimapenzi kimekatazwa wakati wa kufanya I'tikaaf kulingana na maafikiano ya wanavtuoni. Kwahivyo ni jambo la kueleweka inapotajwa neno la "masaajid" kuwa maana ni "I'tikaaf" haitokuwa sawa isipokuwa kwenye Masaajid."

Na 'Aaisha (رضي الله عنها) amesema: "Sunnah ya mwenye kufanya I'tikaaf ni kwamba hafai kutoka nje (ya Masjid) isipokuwa patakuwa na dharura ya kufanya hivyo ambayo inayomlazimu. Hafai kuhudhuria mazishi, asimguse mkewe, wala kuingiliana nae. Na hakuna I'tikaaf isipokuwa kwenye Msikiti unaoswaliwa swala ya Jamaa'ah. Na Sunnah ya mwenye kufanya I'tikaaf ni kwamba anatakiwa awe amefunga swaumu (katika siku atakapofanya I'tikaaf). Msikiti huo vilevile utatakiwa usimamishe swala ya Ijumaa ili asilazimike kutoka hapo Msikitini akaswali swala ya Ijumaa kwengine, kwa sababu kutoka na kuelekea Msikitini ni waajib kutokana na hadeeth ya 'Aaisha katika riwaya yake iliyotangulia: "… na hakuna I'tikaaf isipokuwa kwenye Msikiti unaoswaliwa Swala ya Ijumaa." Zaidi ya hayo ni kwamba nilikuta hadeeth iliyo swaheeh inayoeleza

(Endelea kutoka Uk.. 3)

waziwazi kuhusu neno “Masaajid” iliyowahi kutajwa katika aya hiyo iliyotangulia kumaanisha Misikiti Mitatu: Masjid Al-Haraam, Masjid An-Nabawee na Masjid Al-Aqsaa. Na hadeeth yenyewe ni: “Hakuna l’tukaaf isipokuwa kwenye Misikiti mitatu.”
Kulingana na niliyowahi kuyaona, wale miongoni mwa ma-Salaf wenye kuishikilia rai hii ni Hudhayfah Ibn Al-Yamaan, Sa'eed Ibn Al-Musayyib na 'Ataa. Lakini hatahivyo, (Ataa’) hakutaja Masjid Al-Aqsaa. Wengine wakashikilia rai yakwamba ni Msikiti wowote unaoswaliwa swala ya Jamaa’ah (na ambao swala ya Ijumaa inaposwaliwa), bila ya kizuizi chochote. Lakini wengine wakakataa na kusema yakwamba inaweza kufanyika hata kwenye msikiti wa nyumbani kwake. Na hapana shaka yakwamba kushikamana na linaloafikiyana na hadeeth kuhusiana nayo ndilo lenye kustahiki kufuatwa, na Allaah (سبحانه وتعالى) ndiye Mjuzi zaidi.

Ni katika Sunnah kwa mwenye kufanya l’tikaaf awe amefunga kama ilivyoelezwa na ‘Aaisha (رضي الله عنها). Amepokea al-Bayhaqee kutoka kwa Ibn Abbaas yakwamba alisema: “Kwa hakika mambo ya kuchukiza mbele ya Allaah ni mambo ya Uzushi. Na kutokamana na mambo ya kuzua ni huku kufanya l’tikaaf kwenye Masaajid yaliyo kwenye majumba.” [Imepokewa na Al-Baihaqee kwa silsila ya upokezi iliyo swaheeh na Abu Daawood kwa silsila nzuri ya upokezi]. Imaam Ibn al-Qayyim amesema katika Zaad Al-Ma'aad: "Haikupokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba ati alifanya l’tikaaf akiwa hakufunga. Bali, ‘Aaisha (رضي الله عنها) amesema: “Hakuna l’tikaaf isipokuwa kwa aliyefunga.” Na zaidi ni kwamba Allaah hakuitaja l’tikaaf isipokuwa pamoja na kufunga. Na Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuifanya isipokuwa alikuwa amefunga. Kwahivyo rai ya sawa iko kwenye dalili ambayo wanavyuoni wengi wameshikamana nayo; yakwamba kufunga ni miongoni mwa shuruti za l’tikaaf. Na hii ndiyo rai aliyojichagulia Sheikh ul-Islaam Abul ’Abbaas Ibn Taymiyyah.

YENYE KURUHUSIWA KWA MWENYE KUFANYA I’TIKAAF:

1. Anaruhusiwa kuondoka Msikitini kwa min-ajil ya kutekeleza mahitaji yake. Vilevile anaruhusiwa kutokeza kichwa chake nje ya Msikiti ili kipate kuoshwa na kuchanwa. ‘Aaisha (رضي الله عنها) amesema: “Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliingiza kichwa chake nilipokuwepo na yeye alikuwa akifanya l’tikaaf Msikitini, na mimi nilikuwa kwenye chumba changu. Basi nilikuwa nikimchana nywele zake [na kwenye riwaya moja: niliziosha, hata ingawaje palikuwa na kizingiti baina yetu, na mimi nilikuwa kwenye ada yangu ya mwezi], na yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa haingii chumbani kwangu mpaka akiwa na haja ya dharura alipokuwa akifanya l’tikaaf.”
2. Inaruhusiwa kwa mwenye kufanya l’tikaaf na wengine watawadhe msikitini, kutokana na hadeeth ya aliyekuwa akimtumikia Mtume (صلى الله عليه وسلم): “Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akitawadha kwa wudhoo’ mwepesi msikitini.”

SERANI [ARAB-BOYS] SPORTS GROUND

HILI NI TANGAZO KWA NDUGU ZETU WAISLAMU, WAKE/WAUME YAKWAMBA, TUTASWALI SWALA YA ‘EID UL-FITR KATIKA UWANJA WA SERANI [ARAB-BOYS] SPORTS GROUND PINDI MWEZI UTAKA-POSHUHUDIWA MAHALI POPOTE KATIKA ULIMWENGU MZIMA. TWAMUOMBA ALLAAH AZITAKABALI SAUMU ZETU NA ATUSAMEHE MAD-HAMBI YETU NA ATUINGIZE PEPONI.

3. Anaweza kutengeneza hema dogo nyuma ya Msikiti ambao anapofanya l’tikaaf. Kwa vile ‘Aaisha (رضي الله عنها) alikuwa akimtengenezea Mtume (صلى الله عليه وسلم) Khibaa anapofanya l’tikaaf. Na hii ilikuwa ni amri yake (صلى الله عليه وسلم). Wakati mmoja alifanya l’tikaaf kwenye hema moja dogo lililokuwa limefunikwa na mkeka kwenye mlango wake.

KURUHUSIWA MWANAMKE KUFANYA I’TIKAAF NA KUMZURU MUMEWE [ANAYEFANYA I’TIKAAF MSIKITINI]:

4 Inaruhusiwa kwa mwanamke kumtembelea mumewe akiwa (huyo mume) anafanya l’tikaaf. Na anaruhusiwa kutembea naye kwa ajili ya kumshindikiza mpaka mlangoni, kwa kuitegemea hadeeth ya Swafiyyah (رضي الله عنها): “Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifanya l’tikaaf Msikitini katika siku za mwisho za mwezi wa Ramadhaan, basi usiku mmoja nikenda kumtembelea, na alikuwa na wake zake. Nikazungumza naye kwa kiasi cha Saa moja nzima, kisha nikasimama kutaka kuondoka, akaniambia, ’Usiwe na haraka, mimi nitatoka pamoja na wewe.’ Mara akasimama pamoja na mimi ili anishindikize mpaka nje.” Naye (Swafiyyah) makaazi yake yalikuwa ni kwenye nyumba ya Usaamah Ibn Zayd. Kisha wakaanza kutembea mpaka wakafika kwenye mlango wa Msikiti, uliokuwa pambizoni mwa mlango wa Umm Salamah. Mara wakapita watu wawili miongoni mwa ma-Answaar. Walipomuona Mtume (صلى الله عليه وسلم), wakaanza kutembea kwa haraka zaidi, basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaambia: “Hebu punguzeni haraka zenu! Huyu ni (mke wangu) Swafiyyah Bint Huyay.” wakasema: “Subhaanallaah; Ewe Mjumbe wa Allaah.” Akasema [Mtume (صلى الله عليه وسلم)]: “Kwa hakika Shetwani hutembea ndani ya mwili wa mwana-adamu kama damu inavyopita kwenye mishipa. Na mimi nahofia isije akawatia uovu kwenye nyoyo zenu.” [Au Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema]: “Kitu ndani ya nyoyo zenu.” kwa kweli inaruhusiwa hata mwanamke kufanya l’tikaaf pamoja na mumewe msikitini au peke yake, kwa maneno ya ’Aaisha (رضي الله عنها): Mmoja miongoni mwa wake za Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwahi kufanya l’tikaaf pamoja naye, haliyakuwa kwenye Istihaadhah (akitokwa na damu baina ya siku zake za ada) [katika riwaya nyengine imesema yakwamba alikuwa ni Umm Salamah] naye alikuwa akiona (damu) nyekundu au athari za manjano (zikimtoka). Na mara nyengine tulikuwa tukimuwekea kitasa chini yake wakati alipokuwa akiswali. Na pia alisema: “Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifanya l’tikaaf wakati wa siku kumi za mwisho za mwezi wa Ramadhaan, mpaka kufa kwake. Kisha wake zake wakaendeleza kufanya l’tikaaf baada ya kufa kwake.” Kuna dalili kwa hili yakwamba wanawake wanaruhusiwa kufanya l’tikaaf. Na hapana shaka yakwamba haya ni kwa sharuti yakwamba wasimamizi wao wawakubalie kufanya hivyo. Na pia kwa sharuti yakuwa mahali penyewe pasiwe na fitna yoyote na kutangamana na waume, kutokana na dalili chungu nzima na pia chini ya misingi ya ki-Fiqh:

KUZUIYA MAOVU HUTANGULIZWA KULIKO KULETA MAZURI

[ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO]